# ANGAZA NURU YAKO

## shuleni & nyumbani



Mch. Denis & Devis Julius

## Utangulizi:

Huu ni mwendelezo wa miongozo ya mafunzo ya Watoto, Ni vema kama mzazi/ mlezi / Mwalimu wa Watoto, ujue kuwa moja ya agizo la Bwana Yesu, ni sisi kuiangaza Nuru yetu kwa ulimwengu, Na wajibu huu sio kwa watu wazima tu, bali kwa watu wote (yaani Watoto na watu wazima). Tukiwafundisha Watoto wetu mapema tangu wakiwa wadogo jukumu hili, halitawasumbua kukua nalo hadi uzeeni. Licha ya kuwa Mungu atatukuzwa mioyoni mwao kwa kufanya hivyo , lakini pia watafanyika msaada kwa makundi mengi yetu watu kumwona Mungu.

Mara nyingi tunafikiri, kumuangaza Kristo, ni lazima iwe kuhubiri, lakini kwa njia ya matendo yetu mazuri, Kristo anajulikana mbele za watu kwa kasi zaidi. Hivyo darasa hili, limeegemea kumjenga mtoto awapo katika maeneo mawili ambayo sehemu kubwa ya maisha yake huegemea. Eneo la Kwanza Ni SHULENI, na Eneo la pili ni NYUMBANI.

Baada ya mafunzo haya mtoto ataweza, kujua na kueleza kwa ufahamu sahihi;

Yeye ni Nuru kwa namna gani awapo shuleni na Nyumbani

Mathayo 5:14-16

*14 Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima.*
*15 Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango; nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani.*
*16 Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.*

Zingatia: Ili kupata miongozo mingine ya nyuma ya madarasa ya Watoto wasiliana nasi kwa namba uzionazo mwisho kabisa mwa Makala hii, Bwana akubariki.

~Mch. Denis & Devis Julius.

# NURU NI NINI?

**Mwl:** Kabla hujawafundisha kinadharia wafundishe kivitendo. Wapeleke kwenye chumba chenye giza kabisa, funga milango na madirisha yote, kisha waulize, je mnaona nini katika giza hili? (Watakujibu na kusema hatuoni chochote). Kisha chukua tochi, au washa taa, tena waulize, kila mmoja je! Mnaona nini? Watakujibu ndio, watasema tunaona vitu mbalimbali, vitabu vyetu, mapazia, meza, nguo, lakini pia tunaonana sisi kwa sisi n.k.

**Mwl:** Baada ya hapo waambie vivyo na hivyo na sisi tunaitwa Nuru ya ulimwengu ili kuwasaidia wengine kumwona Mungu kupitia maisha yetu.

**Mwl:** Utawauliza Watoto, ikiwa taa, itafichwa chini ya uvungu, Je itaweza kumulika vema ndani vitu vikaonekana?

**Watoto:** Watajibu Hapana

**Mwl:** Waambie, vivyo hivyo na sisi hatupaswi kuyaficha matendo yetu mema, bali tunatakiwa tuyadhihirishe waziwazi kwa watu ili wasaidike kumjua Mungu.

**Mstari wa Kukariri:**

Mathayo 5:16 *Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.*

## Matendo yapi mtoto ayafanye awapo shuleni :

Haya ni mambo ambayo kama mwalimu, umfundishe mtoto kila awapo shuleni, , kwasababu huko ndiko karakana yake ya matengenezo ilipo, asipoangaza nuru ya Kristo, kinyume chake ni kuwa shetani atamsaidia kutandaza giza. Hakuna mahali pa kati, hivyo usipuuzie kumjengea maadili mapema:

1. **Kupatanisha.**

Mfundishe kwa kumwambia anapoona wenzake wanapigana, awe wa kwanza kutatua ugomvi, na kuwafanya wakae Pamoja tena, Halikadhalika pale wenzake wanapomchokoza au kumuudhi, aipuke magomvi hayo aidha kwa kukaa kimya au kwa kuondoka mahali pale, au kwa kutoa taarifa kwa waalimu. Akitenda hivyo wanafunzi wenzake watajua kuwa Mungu ni mpatanishi, na kamwe hapendezwi na magomvi na mashindano, matokeo yake itakuwa ni wao kuzijua tabia za Mungu.

2. **Kuzungumza**

Eneo la pili ni mazungumzo, mfundisha ajifunze kutumia maneno ya heshima, kama vile kusema asante, pale anaposaidiwa, kusema samahani pale anapokosea, kuepuka matusi. Akijifunza kuwa na maneno heshima na staha, watajua watu kuwa Mungu ni hufurahishwa na adabu huwafanya watu kuwa na adabu nzuri, Na matokeo yake watatamani kumfuata Kristo na wao wawe vivyo hivyo.

3. **Kusaidia Watoto  wengine**

Mfundishe kusaidia wenzake kuelewa darasani, pale ambapo hajaelewa awe wa kwanza kusaidia kuelewa, anapoona mwezake ana njaa, akaja kumwomba na yeye anacho kidogo asimnyime mwenzake,. Anapoona mwanafunzi mwenzake ametengwa na wengine kwasababu hana akili, aende kumfariji. Akifanya hivyo watajua kuwa ni kweli Mungu ni wa rehema, na upendo, kwasababu anawafanya Watoto wake pia kuwa vivyo hivyo.

4. **Usafi**

Wafundishe kuwa Yesu hapendezwi na uchafu, Na pale wanapokuwa wasafi, watu watatambua kuwa Mungu hakai mahali pachafu.  Hivyo ajifunze kuwa msafi wa mwili, kwa

kuoga, kufua nguo, kukata kucha, na kuchana nywele zake. Ili Mungu asionekane, hajali watu wake.

5. **Kuwa na bidii**

Wafundishe kuwa wapanaswa Kumaliza mazoezi ya shuleni (Home Works), kuzingatia kusoma kwa bidii, mwambie mtu anapokuwa na ufaulu mzuri, basi wenzake watathibitisha kuwa Mungu huwafanyi watu kuwa wajinga, bali vichwa sawasawa na Neno lake. Na matokeo yake ni kuwa watavutiwa kwa Kristo.

6. **Heshima**

Wafundishe, kuwaheshimu waalimu shuleni na wazazi, iwe ni sehemu ya maisha yao ya kila siku, wanapoona wenzao wanawasema vibaya waalimu, wasikubali kuungana nao. Wakifanya hivyo Watoto wenzao watajua kuwa Mungu hupendezwa na heshima. Kama vile Yesu alivyowatii wazazi wake. Na wao pia wakitaka kuja kwa Kristo watapata picha ya utii.

## <u>Wimbo wa kukariri:</u>

Wafundishe, aidha wimbo mmoja/ miwili ya kukariri, wimbo huo waweza kuwa tenzi ya Rohoni au sifa, au wa kuabudu,

wenye maudhui ya  sisi tufanyike nuru ya ulimwengu, tufanane na Kristo.

Kwamfano waweza wafundisha wimbo wa kuabudu unaosema.. “Natamani kufanana nawe, sikuzote za maisha yangu,”

**<u>Zoezi:</u>**

Wapangilie Watoto, mpe kila mmoja jukumu la kwenda kulifanya wiki hii. Anza kwa kuwauliza ni wapi ambapo hawakuzingatia kufanya, au pamekuwa pagumu kupatekeleza, kisha mwambie akapafanyie kazi wiki hii, ili ajapo wiki ijayo akupe mrejesho alitenda nini cha ziada, je ni kuonyesha heshima kwa wazazi & waalimu, au kudumisha usafi, au masomo, au kupatanisha, au kusaidia?

Zingatia: Wiki ijayo kukusanya mrejesho.

**<u>Ukiri:</u>**

Kama Bwana Yesu alivyo nuru, vivyo hivyo na mimi nitafanyika nuru niwapo shuleni, nyumbani na mahali popote. Nitahubiri kwa matendo yangu kwa msaada wa Roho Mtakatifu.

## Mwisho

Wafundishe kusali hivi:

Roho Mtakatifu, kwa neema yako niwezeshe kukua katika matendo mema, kama ulivyokaa na Kutenda juu ya Yesu, umekaa juu yangu pia, Nimeomba na kupokea yote, Amen

## Mawasiliano:

Kwa miongozo ya nyuma/maswali/ sadaka

Tel: +255693036618 / +255789001312

Email: info@wingulamashahidi.org

Website: https://wingulamashahidi.org